

STEGA ASSESSMENT TEST - GREDI YA 4 2020

COMPETENCY BASED CURRICULUM



SHUGHULI ZA LUGHA

JINA: _____

SHULE : _____

MUDA : SAA 1 DAK 40

1. Taja vifaa shambani (alama 2)



a) _____

b) _____

2. Chora na upake rangi vifaa viwili vya shambani. (alama 2)

a) _____

b) _____



3. Jaza pengo kwa kuchagua jibu sahihi. Kumbuka si lazima utumie majibu yote.
(alama 5)

(udaktari, useremala, urubani, uchuuzi, ususi, ukulima, upishi, utaratibu, ualimu, udereva)

a) Kazi ya _____ ni ya kutibu wagonjwa.

b) Augustine amefanya kazi ya _____ wa matatu kwa miaka mingi.

ch) Masoko mengi yamejaa watu wanaofanya kazi ya _____




e) Nikitaka kusuka watu nywele nitajifunza kazi ya _____

f) _____ ni kazi ya kutengeneza vitu kama meza kwa kutumia mbao.

4. **MADA: UZALENDO (alama 3)**

Mada: Kuandika

Andika jina sahihi la mchoro



5. **Kamilisha kifungu hiki kwa kutumia maneno yafuata. (alama 10)**

Likizo ya muhula wa tatu ni ndefu. Likizo hii huanza Novemba hadi 1. Mwezi wa 2 huwa na sherehe nyingi sana. Watu husafiri ili kuwa na familia zao.

Wazazi hujiandaa kuwapeleka watoto shuleni 3. Wazazi huwanunulia watoto wao vitabu na pia kulipa karo. Watoto huenda shule Januari, 4 na 5. Muhula wa kwanza unapoisha wanafunzi huenda likizo mwezi wa 6.

Siku ya wafanyikazi huwa 7 huku sikukuu ya madaraka ikiwa mwezi wa

10.

(Mei, Juni, Disemba, Januari, Februari, Machi, Aprili)

6. **Jaza nafasi ukitumia haraka au polepole. (alama 4)**

a) Nikitembea _____ nitachelewa.

b) Ukila chakula _____ kitakunyonga.

ch) Niliendesha baiskeli _____ ili nifike nyumbani mapema.

d) Nilitembea _____ kwa matope ili nisianguke.

MADA : NDEGE NIMPENDAYE

7. MADA NDOGO: NDEGE WA NYUMBANI

Andika malina ya ndege watano wa nyumbani unagowajua. (alama 5)

- a) _____
- b) _____
- ch) _____
- d) _____
- e) _____

8. Tumia -na-, -li-, -ta- kujaza mapengo. (alama 5)

- a) Yeye a ___ piga deki sasa.
- b) Katana a ___ palilia shamba langu kesho.
- ch) Wao wa ___ panda miti jana.
- d) Wanafunzi wa ___ enda shuleni kesho.
- e) Mwalimu mkuu a ___ funza wanafunzi sasa.

9. Soma ufahamu ufuatao kisha ulibu maswali. (alama 10)

Mwalimu wetu alitupeleka soko la Kongowea siku moja asubuhi. Tulizuru vibanda tofauti. Kuna vibanda vilivyouza mboga kama vile sukumawiki, kabeji na karoti. Vibanda vingine viliuza matunda kama vile machungwa, ndizi na maembe.

Kabla ya kuuza bidhaa, wauzaji walipima bidhaa kwa kutumia ratili. Wauzaji pia waliwapatia wanunuzi karatasi fulani iliyoitwa risiti. Risiti ilitolewa ili kuonyesha kuwa muuzaji alikuwa amepokea pesa kutoka kwa mnunuzi.

Tulipita mahali kwingine ambako tulimsikia mtu akitangaza bei za bidhaa kwa sauti mbele ya watu. Watu waliokuwa hapo walishindania bidhaa hizo. Mwalimu alitueleza

kuwa huo ulikuwa mnada na aliyekuwa anatangaza bidhaa alitwa dalali.

Maswali

- a) Mwalimu aliwapeleka wanafunzi soko lipi? _____
- b) Wauzaji waliuza mboga zipi kwenye vibanda? _____
- ch) Wauzaji walipima uzito wa bidhaa kwa kutumia kifaa kipi? _____
- d) Mwuzaji alipatia nini mnunuzi ili kuonyesha kwamba amepokea pesa zake?

- e) Mtu aliyekuwa alitangaza bidhaa alitwa _____
- f) Taja tunda moja ambalo lililouzwa kwenye vibanda. _____
- g) Mwandishi na wenzake walipelekwa sokoni na nani? _____
- h) Je, kabla ya kuuza bidhaa, wauzaji walifanya nini? _____

10. **Jibu maswali yafuatayo kwa kutumia -ake na -ao. (alama 4)**

- a) Kila mzalendo hujivunia nchi y _____
- b) Wanafunzi hutumia penseli z _____ kuchora.
- ch) Taifa lenye maendeleo hujali maslahi ya raia w _____.
- d) Wakimbiaji hutumia vipawa vy _____ kukimbia.

Viwango vya kutathmini

Kuzidisha Matarajio	Kufika Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
48 - 50	40 - 47	30 - 39	0 - 29